



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO



Kumb. Na. HW/A/S.50/22/VOL.II/123

01/03/2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo anakaribisha maombi ya Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi mbili kupitia Kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb. Na. FA.170/358/01"C"/137 cha tarehe 13, Januari, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III - NAFASI 02

SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji anatakiwa awe na cheti cha kufaulu Kidato cha Nne (IV) na waliohitimu mafunzo ya Cheti (Astashahada) katika fani zifuatazo: Utawala, Uongozi na Usimamizi wa Fedha, Sheria, Elimu ya Jamii, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo/Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU

- I. Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- II. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- III. Kiongozi wa wataalamu (watumishi wa serikali) katika kijiji.
- IV. Mhasibu (Afisa masuuli) na Mtendaji Mkuu wa kazi za kila siku za Serikali ya Kijiji.
- V. Kutafsiri na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Taratibu zinazotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- VI. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
- VII. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.

- VIII. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- IX. Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na Mwajiri.
- X. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

MSHAHARA


Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani ngazi ya Mshahara wa TGS B.

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- I. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania.
- II. Waombaji wawe na umri wa kuanzia miaka 18 na wasizidi miaka 45.
- III. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- IV. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- V. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- VI. Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni landikwe jina kwa nyuma.
- VII. Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", Hati Matokeo za Kidato cha Nne na Sita, yaani FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS HAVITAKUBALIWA.
- VIII. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 14, Machi, 2023 saa 9:30 Alasiri.
- IX. Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili fasaha au Kiingereza fasaha na yatumwe kupitia Posta kwa anuani ifuatayo:

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO,
S.L.P 43,
KIBONDO**

IMETOLEWA NA:



**Rutema D.M
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KIBONDO**



Kibondo, S.L.P. 43, Kibondo- Kigoma, Simu: +25528-2820084 , Nukushi +25528-2820084,
Barua pepe: ded@kibondodc.go.tz Tovuti: www.kibondodc.go.tz

[Barua zote zilandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)]